# *NAPIGA MAGOTI NIKUABUDU*

*Frt. Aidanus Chimazi*
*Segerea Seminari*
*27/11/2021*




2. Napiga magoti mbele yako,
Maskini m-tupu nikiomba,
Neema pia huruma yako,
Kwa mwangao fukuza upofu (upofu),
Na moyo wangu uvutwe kwako.

3. Mostransioni humo ulimo,
Unang`aa mithili ya jua,
Jua linavyoangaza pote,
Uangaze na rohoni mwangu (Mwa-ngu)
Mwanga wa kweli na nuru yako

4.Nuru iangazayo zaidi,
Kuushinda mwanga wa mchana,
Ni nuru gani angavu hii?,
Kwa mkali zaidi mwangaza, (mwangaza)
Nayo yang`ara kama dhahabu.

5. Mmimino wa neema zako,
Usipite mbali nami Bwana,
Bali moyoni mwangu upenye,
Zijae kwa wingi ndani mwangu, (mwa-ngu)
Zinisaidie kuja kwako

6. Na mwisho mbinguni nifikie,
Nimtukuze Baba na Wewe,
Pamoja na Roho Mtakatifu,
Watakatifu na Malaika, (kasote)
Tukiisifu adhama yako.

7.Tunakuomba hayo Ee Yesu,
Unayeishi na kutawala,
Pamoja na Baba naye Roho,
Ni Mungu `moja hata milele, (milele)
Milele na milele. Amina